



ISO 9001:2015 CERTIFIED

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



USHIRIKA

Afya

Uhakika wa Matibabu kwa Wote

TOLEO LA MEI 2021

 www.nhif.or.tz

 Piga **0800 110063** bure

   [nhifz](#)

 [NHIF ONLINE TV](#)

USHIRIKA AFYA

(Bima ya Afya kwa Wakulima na Wafugaji)

Ushirika Afya ni mpango wa bima ya afya kwa wakulima na wafugaji walio kwenye vyama vya ushirika vya msingi vilivyosajiliwa. Mpango huu unawapa urahisi wa kupata huduma za matibabu kwa kuchangia kabla ya kuugua. Huduma hizo zinapatikana katika vituo vya matibabu zaidi ya 9,000 vilivyosajiliwa na NHIF nchi nzima.

WALENGWA/ WANUFAIKA

Mpango wa USHIRIKA AFYA unawalenga wafugaji na wakulima mbalimbali nchini ambao ni wanachama katika vyama vya msingi vya ushirika pamoja na wenza wao na watoto wao.

MAFAO YATOLEWAYO

Wanufaika wa USHIRIKA AFYA watapata huduma za msingi na za kibingwa katika vituo vya matibabu kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali za rufaa za Taifa ikijumuisha vituo vya Serikali, Mashirika ya dini na Binafsi.

Mafao hayo ni:-

- Kujiandikisha na kumwona daktari
- Dawa
- Vipimo
- Kulazwa
- Upasuaji mdogo, mkubwa pamoja na upasuaji wa kujifungua kwa wanawake
- Matibabu ya kinywa na meno
- Matibabu ya macho
- Mazoezi ya kimatibabu ya viungo (physiotherapy)
- Vifaa saidizi kama magongo, vishikizi vya shingo

JINSI YA KUJIUNGA NA MICHANGO

- Chama cha ushirika cha msingi kitaingia makubaliano na NHIF kwa kujaza fomu maalum,
- Usajili utafanyika kwa pamoja kwa makundi ya wanachama wasiopungua 100 wa chama husika.
- Mwanachama wa chama hicho atajaza fomu maalumu ya kujisajili. Fomu hiyo itakuwa na taarifa zake na wategemezi wake anaotaka kunufaika nao.
- Mwanachama atachangia Tsh. 76,800 kwa mwaka kwa kila mnufaika.
- Chama kitakuwa na wajibu wa kukusanya fomu na michango ya wanachama wake wanaojisajili na NHIF na kuiwasilisha katika Mfuko.
- Mwanachama atapatiwa kadi ya NHIF ambayo ataitumia kupata huduma za matibabu katika vituo vilivyosajiliwa na Mfuko nchi nzima.

Kujisajili kwa Kuwezesha na Taasisi za Fedha:

Chama cha msingi kina fursa ya kuingia makubaliano na taasisi za fedha ambapo wanachama hulipiwa michango ya NHIF na taasisi za fedha zilizoingia makubaliano na NHIF kwa mikopo isiyo na riba itakayorejeshwa baada ya mavuno.

Huduma kwa Wateja Piga Simu bila Malipo
0800 110063